

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA THELATHINI NA TISA**

**02 JUNI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA TISA – TAREHE 02 JUNI, 2023

#### I. DUA:

#### II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

#### WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

#### MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **501. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna Mwongozo unaoruhusu Watu Wenye ulemavu mmoja mmoja kukopeshwa fedha za Halmashauri.

##### **502. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Sheria italetwa kupunguza michakato ya utangazaji wa Miradi ya TARURA na fedha kusimamiwa na Mameneja wa Wilaya.

##### **503. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itawapa ajira za kudumu Walimu walioajiriwa tangu Mwaka 2002 kwa masharti ya ajira za muda Ulyankulu.

### **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

#### **504. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaboresha Madaraja ya Kampimbi na Mgandu Wilayani Same.

#### **505. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Barabara ya Makongolosi - Mkiwa - Chunya itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

### **WIZARA YA KILIMO:**

#### **506. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kwa nini Serikali isiruhusu Wafanyabiashara wazawa wa kusindika Kahawa Mkoa wa Kagera kununua kutoka kwa Wakulima.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**507. MHESHIMIWA KATANI AHMAD KATANI (TANDAHIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itapeleka mawasiliano ya simu yenyewe usikivu katika Kata za Litehu, Ngonja na Mkwiti Wilayani Tandahimba.

**508. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, kwa kiasi gani Mkongo wa Taifa umesaidia kuboresha na kupunguza gharama za mawasiliano.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **509. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha matawi ya Vyuo Vikuu vya Umma katika Mkoa wa Katavi.

### **510. MHESHIMIWA OMAR ALI OMAR (WETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kwa nini Serikali haipangi kusahihishia Mitihani ya Kidato cha Nne Zanzibar.

## **WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

### **511. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, kwa nini Serikali inapotwaa maeneo ya Wakulima isiwatenggee maeneo mengine licha ya kulipa fidia.

**512. MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT  
MATHIAS GWAJIMA (KAWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itamaliza migogoro ya ardhi maeneo ya Chasimba, Chatembo, Chachui, Nkasangwe na Mabwepande - Kawe.

**WIZARA YA AFYA:**

**513. MHESHIMIWA JUDITH SALVIO KAPINGA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali inafanya nini kuhakikisha uviaji mimba usio salama unakwisha.

**WIZARA YA NISHATI:**

**514. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO  
DAVID (SAME MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ahadi ya Serikali ya kusambaza umeme wa REA III katika Vijiji 48 vya Jimbo la Same Magharibi na Vitongoji vyake imefikia wapi.

## **515. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme katika Kata za Lagana, Itilima na Bunambyu Wilayani Kishapu.

### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupidisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA  
02 JUNI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**